

Maswali

1. Mungu alifanya nini ili nchi ionekane mzuri?
2. Mungu alifanyia Adamu na Hawa nini?
3. Mungu alikataza Adamu na Hawa wasifanye nini?
4. Hawa alikutana na nini karibu na mti wa ujuzi wa mema na mabaya?
5. Nyoka alisema uongo gani?
6. Adamu na Hawa walifanya kosa gani?
7. Mungu alijisikiaje wakati Adamu na Hawa hawakumtii?
8. Nyoka aliadhibiwa namna gani?
9. Adamu na Hawa waliadhibiwa namna gani?
10. Nani alisimama karibu kwa lango la Bustani ya Edeni?

Majibu

1. Mungu alifanya mwangaza, hewa, jua, mwezi na nyota, nyasi na maua na miti, ndege, samaki, wanyama na mtu – Adamu na Hawa.
2. Mungu aliwafanyia Adamu na Hawa bustani nzuri ya kuishi ndani.
3. Lazima wasile tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya.
4. Hawa alikutana na nyoka.
5. Nyoka alisema uongo, “Hakika hautakufa.”
6. Walikula tunda la mti wenye Mungu aliwakataza wasikule.
7. Mungu alikasirika sana.
8. Nyoka alitambaa kwa tumbo na kukula mavumbi.
9. Watafanya kazi kwa nguvu halafu wakue wazee na wafe. Waliondoshwa kwa Bustani nzuri ya Edeni.
10. Malaika alisimama langoni na upanga wa moto uliogeuka pande zote.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



1 Bustani ya Edeni

Marejeo

Mwanzo mlango 2: 4 – 25 na mlango wa 3

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu aliumba nchi nzuri na bustani ya kupendeza ili Adamu na Hawa waishi. Lakini Adamu na Hawa hawakupenda Mungu kamili kwa hivyo waliondoshwa.

Maneno maalum

- 1.1 Mungu aliumba + nchi na anga + mzuri + mwangaza + hewa + jua, mwezi na nyota + nyasi, miti na maua + ndege na samaki + wanyama + mtu + Adamu na Hawa
- 1.2 Mti wa ujuzi wa mema na mabaya + usile + kufa
- 1.3 Hawa + nyoka + nyoka anasema uongo + hakika hautakufa
- 1.4 Hawa alikula tunda + Adamu alikula + ogopa + Mungu anaita
- 1.5 Mungu ana huzuni + adhibiwa
- 1.6 Nyoka alitambaa kwa tumbo + Adamu na Hawa wafanya kazi + kua wazee na kufa + toka kwa Bustani + malaika + malaika langoni

1.1 Zamani za kale, Mungu alifanya nchi na anga. Mwanzoni kulikuwa na giza kingi nchini, kila siku ilikuwa usiku. Siku moja Mungu aliamua kuifanya nchi ionekane vizuri. Aliamua kuweka mwangaza nchini. Akafanya hewa ili tupumue. Alifanya jua, mwezi na nyota. Mungu alifanya nyasi, miti na maua. Akafanya ndege, samaki na wanyama. Halafu Mungu akafanya mtu aliyeitwa Adamu na mkewe, Hawa.

Mungu alitengeneza bustani nzuri ili Adamu na Hawa waishi ndani. Hiyo bustani ilikuwa na miti mizuri na maua mazuri. Mto ulipita ndani yake. Iliitwa Bustani ya Edeni.

1.2 Adamu na Hawa walitunza bustani na wakaishi kule na furaha kwa sababu Mungu alikuwa amewapa kila kitu walichohitaji. Kuna kitu kimoja chenye Mungu hakutaka wakifanye – lazima wasikule tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya uliokuwa katikati ya Bustani. Mungu alisema kwamba wakikula hilo tunda watakufa.



1.3 Kwa hiyo bustani kulikuwa na nyoka. Siku moja Hawa alikuwa anatembea katikati ya bustani, akakutana na nyoka karibu na mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Nyoka alimuuliza, “Mbona usikule tunda la huu mti?” Hawa alimjibu, “Mungu alitwambia

kwamba lazima tusile tunda la huu mti, tukila tutakufa.” Nyoka alidanganya Hawa, “Hakika hautakufa ukila hili tunda. Itakufanya uwe na akili kama Mungu.”

1.4 Hawa aliangalia hilo tunda likamfurahisha. Akafikiria vile anaweza kuwa mwerefu kama Mungu. Alichuna tunda moja kutoka kwa huo mti na akala. Alichukuwa sehemu ya hilo tunda na akampa Adamu na kumwambia vile nyoka ilisema. Adamu naye alitaka kuwa na akili ikiwa Hawa amekuwa. Kwa hivyo naye alikula hilo tunda.

Baada ya kukula hilo tunda, walikunduwa kwamba wamefanya makosa. Waliogopa sana. Waliposikia sauti ya Mungu ikiwaita, walichificha nyuma ya miti bustanini.

1.5 Mungu alikasirika sana alipokundua kwamba wamekula tunda alilo katasa wasikule. Mungu alikuwa amewapa kila kitu walichotaka. Alitumainia kwamba watamtii na kufanya vile amewaagiza. Wote walikuwa wamekosa kwa hivyo wote waliadhibiwa.

1.6 Mungu aliambia nyoka kwamba atatembea kwa tumbo na atakula mavumbi kwa maisha yake yote. Hiyo ndiyo sababu nyoka anaenda kwa kujinyonga nyonga chini. Mungu aliambia Adamu na Hawa kwamba wataondoka kwa bustani nzuri na waende kwa ulimwengu. Watafanya kazi kwa bidii ili waguze chakula cha kuwatosha ili wale. Watakua wazee na hatimae watakufa vile Mungu alikuwa amewambia.

Adamu na Hawa waliondoka kwa bustani wakiwa na huzuni. Mungu aliweka malaika na upanga wa moto langoni mwa Bustani ya Edeni ili iwazuia wasirudi ndani.